BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi – Tarehe 27 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mjumbe wa Kamati ya Wabunge Watano Wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

Ripoti ya Wajumbe watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

170. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kujenga masoko mbali mbali nchini ikiwa ni pamoja na soko la Dunga lililojengwa jirani na Skuli ya Msingi na Sekondari ya Dunga. Hata hivyo, ujenzi wa soko hilo haujapokelewa ipasavyo na wananchi.

(a) Je, kuna sababu zipi zilizopelekea Wizara yako kuamua kulijenga soko hilo katika eneo lililopo badala ya kulijenga katika eneo lililochangamka kibiashara kama ilivyo katika eneo la Mitini au Kidimni njia ya Ubago.

(b) Je, Wizara yako imepokea makusanyo ya kiasi gani ya mapato kutokana na soko hilo tokea lilipozinduliwa na

kufanya kazi hadi sasa.

(c) Kwa nini muitiko wa wananchi na wafanyabiashara ni mdogo katika soko hilo, kinyume na ilivyokusudiwa.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

22. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, Zanzibar imenufaika katika maeneo gani kupitia Diplomasia ya Uchumi.

65. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Skuli binafsi zimekuwa na mchango mkubwa katika kutoa elimu na maendeleo yake yanaonekana wazi hapa kwetu Zanzibar. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuhusiana na wingi na ukubwa wa kodi na tozo ambazo skuli binafsi hulazimishwa kutoa bila ya kuangalia mapato na matumizi yake.

(a) Je, ni kodi na tozo za aina gani na za kiasi gani skuli binafsi zinalazimika kutoa.

(b) Je, ni ipi mantiki ya kuzitoza kodi skuli binafsi ilhali zinaisaidia Serikali katika kutoa na kuboresha huduma za elimu nchini.

(c) Je, ni kwa mambo gani na kwa utaratibu upi skuli binafsi zinaweza kupatiwa msamaha katika tozo na kodi za Serikali.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Pango la Kumbi ni miongoni mwa maeneo ya kihistoria yaliyoleta mageuzi makubwa ya asili ya uwepo wa mwanadamu visiwani Zanzibar pamoja na wanyama mbali mbali adimu.

Je, ni kwa njia na mikakati gani inayoichukua Wizara yako katika kulitangaza pango hili kitaifa na kimataifa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

9. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa kumekuwa na mchakato wa mabadiliko ya mitaala ya elimu.

Je, ni kwa kiasi gani mabadiliko hayo yamezingatia dhana ya uchumi wa buluu.

175. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupiga marufuku 'Boarding' kwa wanafunzi wa Darasa la nne kwa skuli zote za Serikali na skuli binafsi hapa nchini. Hata hivyo, katika utekelezaji wa suala hili, kuna fununu kuwa, bado zipo baadhi ya skuli za binafsi zinaendelea kuwaweka 'Boarding' wanafunzi wa Darasa la nne katika skuli zao na kuwataka wazazi wa wanafunzi hao kuchangia kima fulani cha fedha katika kufanikisha 'Boarding' hizo.

(a) Je, taarifa hizi za kuwepo kwa baadhi ya skuli za binafsi zinazoendesha 'boarding' kwa kificho, zimewafikia katika Wizara yako.

(b) Je, Wizara yako inalifuatilia vipi katazo lake hili, ili kujiridhisha kuwa linatekelezwa ipasavyo.

(c) Je, kuna skuli ngali za Serikali na binafsi zilizothibitika kudharau katazo hili.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

117. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Napenda kuipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa kudhamini sekta mbali mbali zikiwemo michezo na masuala mengine.

Kwa nini kumekuwa na mwamko mdogo kwa mashirika na makampuni mengine, kuwekeza katika michezo mbali mbali hususani mpira wa miguu.

124. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,

Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, ni kwa utaratibu gani Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (COSOZA), inawasajili wasanii na wabunifu na hatimae kuweza kuwatambua kama ni wafanyabiashara.

<u>Wizara ya Afya:</u>

12. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa suala la mwananchi kupata huduma bora ya matibabu ni jambo la msingi, na kwa kuwa mazingira ya vituo vya afya vya Matumbini na Kibokoni haviridhishi.

Je, ni lini Serika itatenga fedha kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya vituo hivyo.

149. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt Hussein Ali Mwinyi, mnamo tarehe 1/9/2021 alitoa ahadi ya ujenzi wa vituo vya afya katika kijiji cha Mleteni na Tondooni Mtambwe.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa ili wananchi waweze kunufaika na huduma bora za afya katika maeneo yao.

<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>

172. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pamoja na juhudi kubwa na kasi za ujenzi unaoendelea nchini, kumeibuka khofu ya baadhi ya wananchi wenye maeneo yao hasa yaliyopo katika Mkoa wa Mjini Magharibi, wakiyazungushia uzio wa mabati, wakihofia maeneo yao hayo kuchukuliwa na Serikali iwapo yataendelea kuwa wazi.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inaifahamu khofu hiyo.

(b) Je, kuna ukweli upi kwa Serikali kuyachukua maeneo ya wazi ya wananchi katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

61. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ajali nyingi zinazowahusu watoto wanaopakiwa kwenye bodaboda. Hata hivyo, nyingi ya ajali hizo husababishwa na uzembe na matumizi mabaya ya usafiri huo.

(a) Je, sheria inayokataza bodaboda kupakia zaidi ya watu wawili inatafsiri vipi kuhusu upakiaji wa watoto wengi kwenye bodaboda moja kwa wakati mmoja.

(b) Je, kuna muongozo wowote juu ya matumizi ya kofia ngumu (helmets) kwa watoto wanapopanda bodaboda.

(c) Je, ni tahadhari gani Serikali imechukua kupunguza athari za ajali za bodaboda kwa watoto.

176. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kufuatia kupungua kwa kiasi kikubwa tabia ya vijana wanaoendesha vespa kwa fujo, maarufu kama 'T-ONE', sasa kumeibuka tabia ya vijana kuendesha bodaboda kwa msururu, fujo, uzembe na tabia mbali mbali hatarishi katika barabara mbali mbali hapa Zanzibar.

Je, Wizara yako imechukua hatua zipi kupiga marufuku na kuzuia vitendo hivi.

## IV. <u>RIPOTI YA WAJUMBE WATANO WANAOLIWAKILISHA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:</u>

**<u>Mjumbe wa Kamati ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:</u>**

Ripoti ya Wajumbe watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2023/2024



**Zanzibar,**
**27 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**